# HISTORIA FUPI YA ASILI YA JINA NDALA

Tarehe **22 Novemba 1878** Wamisionari hawa wa Afrika walikanyaga Ardhi ya Ndala **kwa mara ya Kwanza** japo ilikua tu ni kama sehemu ya kupumzika wakiendelea na safari yao kuelekea Uganda.

**Mazingira ya Ndala yaliwapendeza**

Ni dhahiri kwamba baada ya kufika kwao ndala kwa mara ya kwanza mazingira ya mahali hapa yalionekana kuwavutia sana.Waliona kuwa ni mahali pazuri, penye mifugo wengi hasa ng'ombe wengi, maziwa mazuri pamoja na mashamba makubwa na yenye rutuba yaliyolimwa karanga na mtama.

Tofauti na maeneo mengine mengi waliyopita tangu mwanzo wa safari zao,Ndala ni moja ya maeneo amabayo mazingira na wakazi wake waliwapendeza sana wamisionari. Kwakuwa shabaha yao wakati huu haikuwa kutafuta mahali pazuri, bali ilikuwa kuifikisha injili huko Uganda, kumbe kesho yake alfajiri iliwalazimu kuamka na kuendelea na safari yao wakipita maeneo ya Nkinga.

***KUFUNGULIWA KWA MISIONI NA PAROKIA YA NDALA***

**Mnamo tarehe 8 Januari 1896 Ndala ikawa parokia ya kwanza katika Jimbo la Tabora**

## Ndala kitovu cha Ukristo Tabora.

Watu au wakazi wa ndala walikuwa wepesi sana kuipokea dini hii (Ukristo) kuliko wale wa maeneo mengine kama ushirombo na maeneo mengine waliyopita.Hii ilipelekea dini hii ya Ukristo kuenea kwa kasi zaidi hapa ndala kuliko kule Ushirombo ambako wamisionari waliingia mapema kuliko Ndala.

Wakati wamisionari walipofika na kujenga nyumba yao hapa Ndala, wenyeji walikua wachache sana, lakini wamisionari walipofika hata watu **wengine walianza kuhamia maeneo haya ya ndala kutoka unyanyembe, Ugogo na sehemu za kaskazini kwakuwa wenyeji walikua wachache.**

Magonjwa ya mifugo kama ilivyokuwa kule ushirombo hayakuwasumbua watu wa ndala.

Wamisionari walipenda elimu, walikuwa radhi kuanza kujenga shule kable ya hata kigango maana walijenga shule ya **Msingi Ndala mwaka 1909** ambayo sasa ni shule ya Mazoezi Isimba

kufungua chuo cha **makatekista** 1928

.

ta wa mabinti wa Maria lilianzishwa chini ya usimamizi wa masista weupe yaani white sisters. Hawa walijulikana pia kama masista wa mama yetu wa Afrika(MSOLA). Hawa walifanyika kama walezi sasa kwa kipindi chote hadi pale walipokuja kukabidhi utawala kwa masista wazalendo.

Mnamo tarehe **31 Agosti 1939** (Miaka 82 iliyopita) masister hawa wa shirika la Mabinti wa Maria waliwasili ndala wakitokea huko Parokia ya Tlawi jimboni Mbulu na kuanza malezi yao hapa ndala kwa ngazi tatu yaani ukandidati,Upostulanti na Unovisi.Kwa Tabora hii ilikuwa nyumba yao ya **kwanza kufunguliwa ikifatiwa** na ile komventi ya Tabora mjini iliyofunguliwa mnamo tarehe 19 Februari 1941.

**CHUO CHA UALIMU NDALA**

Mnamo tarehe 25 Februari 1952, wamisionari walikianzisha Chuo Cha Ualimu cha ndala kikiwa chini ya umiliki wa Kanisa katoliki Jimbo la Tabora.Chuo kilikuwa chini ya kanisa kwa kipindi cha miaka takribani 18 kabla ya kutaifishwa na serikali.

## Kuwasili kwa masista wa upendo wa Mt. Karoli Boromeo

Masista wa upendo wa mtakatifu Karoli Boromeo waliwasili hapa parokiani ndala kuendeleza kazi ya umisionari, wao walijikita zaidi katika idara ya Afya na hata kupewa usimamizi wa Hospitali hii ya misioni ya Ndala.

Hospitali hii ya misheni ya ndala ilianzishwa mnamo tarehe 25 January 1963 na kukabidhiwa chini ya usimamizi wa masista hawa wa upendo wa mtakatifu Karoli Boromeo. Masista hawa ndio masista ambao hadi leo wanaendelea kuisimamia Hospitali hii chini ya umiliki halali wa Jimbo kuu katoliki la Tabora.

Hospitali hii iliyoanzishwa na wamisionari, ilisaidia kuhudumia kiafya watu wengi walioishi kuzunguka maeneo haya ya ndala na pasipo ubaguzi ilihudumia wakristo na wasio wakristo pia kama inavyoendelea kufanya hadi sasa.

Leo hii hospitali hii ya Ndala imekua ikiwafaidia sio tu wakazi wa Ndala bali hata watu kutoka maeneo mengine mengi nje na ndala wamekuwa wakija hapa ndala na kupata huduma zilizobora za kiafya.

Watu wengi wamepata ajira kutokana na taasisi hii ya afya wazawa na wasio wazawa.Vifo vya wamama wajawazito vimepungua sana kutokana na uwepo wa huduma hii hapa ndala. Elimu mbalimbali kuhusu masuala ya afya imekuwa ikitolewa na wafanyakazi wa Hospitali hii, na kwa uwepo wa hospitali hii watu wamepata huduma nyeti zilizohitaji **madaktari bingwa kwa gharama nafuu ambapo kama ingelazimu kuzifuata huduma hizo maeneo mengine tofauti na hapa ndala, kwa hakika ghalama ya matibabu ingekuwa kubwa sana.**

**HISTORIA YA PAROKIA YA MT. YOSEFU, NDALA.(8 Jan. 1896 - 2021)**

Kabla ya kujengwa Misioni, eneo hili lilikuwa chini ya utawala wa Malkia **NTABO**. Upande wa Magharibi alipakana na PUGE (Zamani Mphuge), kasikazini Nyahuwa na upande wa Kusini-mashariki Unambili (sasa Uyui).

- Wamisionari wa kwanza walipita hapa tarehe 20/11/1878 kuelekea Mwanza.

- Tarehe 8/01/1896 walifika rasmi Ndala wakitokea Uyui, wakati huo Ndala ilikuwa chini ya utawala wa Ntabo. Nyumba zilipangwa kwa Mstari tangu Ndala mpaka Budushi.

- Wamisionari waanzilishi: Pd. Antoon Van de Weed (Antoni Wadei) Padre Mkubwa, Pd. Francois Muller (Francisco Mula- Bwana Malole) na Bruda Max (Maksi) wakisindikizwa na Provika, Padri Francois Gerboin (Fransisko Jerebwa).

- Wamisionari walikuatana na Malkia kwa bahati tu na baada ya hali ya hewa kubadilika, walijenga mahema wakiwa safarini kutokea Ngaya – Kahama kuelekeaTabora.

- Tarehe 01/08/1896 walianza rasmi Missioni chini ya Pd. Antoni Van de Weed akiwa na umri wa miaka 25 tu.

  Bruda Max Boether na Pd. Francisco Muller walikwenda kwa Malkia kule KAMPALA, akawakaribisha na kuwapa eneo la Uhemeli lilokuwa wazi iliwajenge Mission yao.

- Mwanangwa (Mjumbe wa Malkia) aliyeitwa Maganga Hemeli Watugulu aliwafurahia sana hao Wamisionari. Tarehe 15/03/1896, Hemeli alifika na mti mzuri mrefu akawapa hao Mapadri iliwatengeneze Msalaba wa kusimika kuonyesha eneo la kuishi na sehemu ya sala.

- Br. Max alijenga Nyumba ndogo ya kwanza yakuishi Wamisionari tarehe 17/08/1896 na ikabarikiwa 01/11/1896 nabaadaye Br. Timothy alifika kumsaidia.
- Kanisa la kwanza lilianza kujengwa Mwezi wa machi 1892 na Kukamilika tarehe 5 Septemba 1892 na lilibarikiwa na Askofu Heneriko Streicher. Lilikuwa la Tembe.
- Kanisa la pili lilijengwamwaka 1899

- Kanisa la tatu lilijengwamwaka 1912 kwa hatua ya msingi, 1914 kanisa hilolilikamilika. Mnamo tarehe 01/08/1915 Kanisa hilo lilibarikiwa na Askofu Heneriko Streicher.

- Mbatizwawa kwanza alikuwa Maganga Watugulu Mwanangwa wa Malkia Ntabo. Alipewa jina la Joseph tarehe 10/08/1896 sikukuu ya Mt. Laurenti shahidi. Mpaka 1898 kulikuwanawabatizwa 115 tu.

IDADI YA MASISTA: 22

IDADI YA MABRUDA: 06

IDADI YA WABATIZWA: inakadiriwa 12,036

Idadi ya vigango: 29

**TAASISI:**

- ❖ Shule ya Msingi Ndala (sasa Shule ya mazoezi Isimba): 1909 (Sasa ipo chini ya Serikali).
- ❖ Chuo cha Makaekista: 1928
- ❖ Mabintiwa Maria: Walifungua Konventi 1931 ( Masista waalimu kwanza wanawake Tanganyika.
- ❖ Chuo cha Ualimu: 1952 (Sasa kiko chini yaSerikali).
- ❖ Hospitali: 1956 White sisters na baadae waliobwa kusimamia – Masista wa Upendo wa Karoli Borromeo 1963.
- ❖ Baada ya Shule ya mazoezi Isimba na Chuo cha Ualimu Ndala, pia Shule za msingi ambazo zilikuwa chini ya Parokia ya Ndala kabla ya kutaifishwa ni

i. Budushi
ii. Wita
iii. Izinga – Hii ilikuwa Middle School ikiwa chini ya Mambezi ya Mt. Goerge.
iv. Upungu – Shule aliyosoma Askofu Mabula na Mihayo
v. Isuna
vi. Kipugala (Sasa ndani ya Parokia ya Busondo).
vii. Mabisilo (Sasa ndani ya Parokia ya Tongi)
viii. Ndekeli (Sasa ndani ya Parokia ya Tongi)

**TAREHE NA BAADHI YA MATUKIO MUHIMU**

- Tarehe 18 Juni 1897 kuliwekwa Mkataba wakumilikishwa eneo na Afisa wa Serikali ya Kikoloni na watu waliokuwa ndani ya eneo walilipwa fidia.
- 1946 – 1970 kilikuwa kipindi cha Mpito kuelekea uhuru na hata Kanisa la Tanzania (Tanganyika), mwaka 1953 maeneo ya Misioni (Vikariati) yalifanywa kuwa Majimbo. Tabora ikawa Jimbo Kuu tarehe 25/03/1953 na Misioni zake zikajulikana kama Parokia.
- Mageuzi ya Mtaguso wa VatikanoII ya Mwaka 1962 – 1965 Misioni ya Ndala ilifanya juhudi kubwa kuelimisha waamini kutumia zaidi lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza dini na baadaye Kiswahili.

ORODHA YA MAPADRE WA PAROKIA YA NDALA

| No | JINA KAMILI LA PADRE | MWAKA KUZALIWA | MWAKAWA UPADRISHO | MWAKA KUFARIKI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pd. Philip LUZIGA | | 17/08/1928 | |
| 2 | Pd. Alois ISIMANGA | | 1937 | |
| 3 | Pd. Ambrose KASEKA | | 1939 | |
| 4 | Pd. Ambrose MHALIGA | | 1942 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Pd. Germinus KASHIDYE | | 1942 | |
| 6 | Pd. Alexander KABEPELE | | 1945 | |
| 7 | Pd. John KABEYA | | 1948 | |
| 8 | Pd. Andrea KAYIKU | | 1948 | |
| 9 | Pd. John MAGANGA | | 1949 | |
| 10 | Pd. Joseph MANOJA | | 1949 | |
| **11** | **Pd. Alphonce NSABI** | | **1950**=Askofu1969-1989 Kigoma. | |
| 12 | Pd. Paschal MAYUNGA | | 1950 | |
| 13 | Pd. John Mageda | | 1952 | |
| **14** | **Pd. Bernard MABULA** | | **1952** =Askofu1969-2007 Singida. | |
| **15** | **Pd. Mateo SHIJA** | | **1954** = Askofu1984-2018 Kahama. | |
| 16 | Pd. Daniel LUZWILO | | 1960 | |
| 17 | Pd. Charles NYAMITI | | 1962 | |
| 18 | Pd. Simon SHIJA | | 1966 | |
| 19 | Pd. Adelard SHIJA | | 1969 | |
| 20 | Pd. Athanasius | | 1971 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | KIYENZE | | | |
| 21 | Pd. Conard BUGEKE | | 1973 | |
| 22 | Pd. Paulo MAPALAPALA | | 1980 | |
| 23 | Pd. John MUNGONI | | 1980 | |
| 24 | Pd. Julius TENGI | | 1990 | |
| 25 | Pd. Cleofas MABULA | | 1992 | |
| 26 | Pd. Sebastian KASHESHI | | 1994 | |
| 27 | Pd. Novatus SAFARI | | 2009 | |
| 28 | Pd. Prudence RWEYEMAMU | | 2011 | |
| 29 | Pd. Andrea LUZIGA | | 2015 | |
| 30 | Pd. Joseph MASANJA | | 2018 | |

**Waseminaristi:** Parokia yetu ya Ndala ina waseminari (Mafrateri) **kumi na moja**,. (kumi wakiwa katika seminari zetu za Teolojia na falsafa, na mmoja akiwa anaenda kujiunga na mwaka wa Malezi)

## MAKATEKISTA

Tokea mwanzo kabisa wamekuwa mstari wa mbele kufundisha dini.

Makatekista nao waliokua wanufaika wa mwanzo kabisa wa imani hii, hawakuwa nyuma pia katika kuhimiza maisha ya wakfu. Tunaona kwamba mapadre wengi wa mwanzo walikuwa ni watoto wa makatekista hao. Hii inaonyesha jinsi walivyokuwa mstari wa mbele si kwa kuhimiza wengine tu bali walianza katika familia zao wao wenyewe.

Tunayo mifano thabiti katika hili kama vile; katekista Paskali Machibya na Bernard Mapalala wa ndala ambao baadae walipelekwa Ussongo.Hawa watoto wao walikua Sista Maria Justina Paskali na Sista Maria Claudia Mapalala. Hawa wote walikuwa masista wa shirika la mabinti wa Maria. Na kwa bahati iliyoje, Sista Maria Claudia Mapalala aliyekuwa na vipaji vingi katika sanaa na muziki, alibahatika pia Kuwa mama mkuu wa shirika nchini mwaka 1988-1993.

Mifano mingine ni hii; Katekista Petro Mayani yenye mwanae alikua marehemu Padre John B. Maganga (1949-2010). Katekista Adelard Nhunde huyu yeye alitoa watoto wawili mapadre ambao ni Padre John Kabeya na kaka yake Padre Ambrose Mhaliga ambaye alibahatika kuwa Gombera wa Kwanza wa seminari kuu ya Kipalapala. Pia Katekista William Nhindilo huyu yeye mwanae alikuwa Padre John Mageda. Katekista Gervas Ndulila yeye mtoto wake ni Padre Athanasi Kiyenze.

Hao ni baadhi tu ya mapadre ambao ni watoto wa makatekista wazawa.Wapo pia mapadre wengine wengi waliohamasika kutokana na wamisionari na vijana wenzao walioingia katika maisha ya wakfu wakati huo kama watakavyoorodheshwa mwishoni mwa kitabu hiki.

Neema hii haikuishia hapo kwani ni habari njema kusikia kwamba parokia fulani imetoa si tu mapadre bali hata maaskofu, karibu nikujuze. Je wajua kwamba jimbo la Tabora limewahi kutoa maaskofu wazawa watatu pekee? Naam, ndivyo ilivyo lakini kinachotupasababu yakuona kua wanandala tumependelewa sana na Mungu ni kwamba, maaskofu hawa wote watatu ni wazaliwa wa parokia hii ya Ndala.

Naam, mababa hao ni Askofu Bernard Mabula aliyechaguliwa kama askofu msaidizi wa jimbo kuu la Tabora tarehe 4 May 1969 na baadae tarehe 25 March 1972 akateuliwa kuwa askofu wa kwanza wa jimbo jipya la Singida, huyu alikuwa mzaliwa wa kigango cha Bugoda parokia hii ya Ndala. Pia Askofu Alphons D. Nsabi, Aliyefanywa kuwa Askofu wa Kigoma tarehe 22 Februari 1970.Na wa tatu ni Askofu Mathew Shija aliyetamkwa kuwa Askofu wa jimbo jipya la Kahama tarehe 26 Februari 1984.

Haya yote yalikuwa ni matunda ya Utume shirikishi uliofanywa na wamisionari hawa hapa parokiani kwetu Ndala. Ndivyo wanavyotualika pia kushirikisha tunu hizi tulizokirimiwa na Mungu kupitia wao kwa watu wengine. Namna tuishivyo isadifu daima

**Padre John Kabeya na kaka yake Padre Ambrose Mhaliga**. Wote hawa walikuwa watoto wa katekista Adelard Nhunde. Mapadre hawa kutoka hapa Ndala walikuwa miongoni mwa wanufaika wa kwanza kabisa wa elimu iliyotolewa na wamisionari. Hawa walibahatika kuwa wasomi wa mwanzo kabisa katika kanisa la Tabora.

Padre Ambrose Mhaliga.Yeye alibahatika kuwa Gombera wa Kwanza mzalendo wa seminari kuu ya Kipalapala. Kama Padre mzawa wa Ndala ni furaha kwa wana Ndala

kuona kwamba tulipendelewa na Mungu aliyeruhusu Gombera wa kwanza mzalendo awe mzaliwa wa Ndala. Ni tokeo chanya pia la Umisionari kwetu hapa Ndala.

Padre John Kabeya. Huyu alikuwa mdogo wake Padre Ambrose Mhaliga. Padre John Kabeya alikuwa miongoni mwa wasomi wakubwa wa mwanzo si tu hapa Tabora bali hapa nchini. Yeye alikuwa ni mtaalamu sana wa Lugha na alibobea sana kwenye lugha ya Kifaransa. Kitu cha kuvutia zaidi kwake ni kwamba; miaka michache baada ya uhuru alikuja Raiswa Guinea na akakutana na rais wa Tanzania wakati huo Mwalim Julias Kambarage Nyerere. Mtu aliyeonekana anaweza zaidi kutafsiri mazungumzo yale baina ya marais wawili na wananchi alikuwa Padre John Kabeya.

Padre Kabeya aliifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Alimudu kufasiri hotuba ya rais wa Guinea na kuiweka katika lugha yakiswahili. Alimudu pia kufasiri hotuba ya Mwalimu Julius K. Nyerere na kuiweka kwenye Lugha ya Kifaransa. Ni furaha ilioje kwa mzazi kuona mafanikio ya mtoto wake?, kadhalika ni furaha ilioje kwa wanandala kuona wazawa wake wanafanikiwa na kuwa kioo kwa jamii kubwa?, tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa neema na baraka zake kwetu wanandala.

**Padre Karoli Nyamiti.** Padre huyu alikuwa mzaliwa wa Ndala Pia. Wengi tunamfahamu kwa namna alivyoipeperusha bendera ya kanisa la Tanzania kimaataifa. Pamoja na Uchungaji mwingine alioufanya, kipekee yeye pia alihudumu kwa muda mrefu kama Mwalimu kwenye taasisi mbalimbali za kanisa. Alifanya utume wake kama Mwalimu ndani na nje ya nchi. Alifundisha Taalimungu seminari kuu ya Mt. Paul – Kipalapala 1976 **-**1981.Badaye akitokea parokia ya Kipalapala kama Paroko alichaguliwa kwenda Chuo kikuu katoliki cha Africa Mashariki (CUEA) huko Kenya kama mwalimu 1984 -2001.

Baada ya kustaafu aliendelea kubakia huko akiendelea kusaidia majukumu mbalimbali kama mwalimu wa teolojia na muziki katika seminari kuu ya shirika la Mitume wa Yesu hadi Novemba 2019. Alibobea sana kwenye muziki Mtakatifu na alipata tuzo kadhaa za utunzi na upigaji bora wa piano huko nchini Ujerumani. Padre huyu ameandika vitabu pia vingi vyenye mafundisho bora ikiwemo kitabu chake maarufu kiitwacho; *African Theology* kilicho beba ujumbe uitwao *Christ Our Ancestor.*

Katika kitabu chake hicho maarufu anamchora Kristo akimfananisha na Mababu wa zamani. Mila na desturi za mababu zetu na namna walivyoishi na kuwa na imani ndivyo anavyoyafananisha maisha adili ya Kristo kwa kanisa. Padre mwanandala huyu katika maisha yake alifanyika kioo kwa watu na mataifa mengi kwa kushirikisha karama mbalimbali alizojaliwa na Mungu.

**Padre philip Luziga.** Padre huyu ni moja kati ya mapadre watatu wazawa wa kwanza katika jimbo zima la Tabora. Alipadrishwa tarehe 17 August 1928**.** Pamoja nae walipadrishwa pia mapadre wawili ambao wao hawakuwa wazawa wa ndala nao ni padre

Raphael Kavula, pamoja na padre Simon Makulumo.Padre huyu(Luziga) alifungua mlango kwa Ndala katika maisha ya wakfu na kufanya vijana wengi kuendelea kuvutika zaidi. Hii imepelekea parokia ya Ndala kuwa parokia iliyotoa mapadre wengi zaidi kuliko parokia zote katika jimbo hili la Tabora hadi kufikia wakati huu.

**Sista Maria Claudia Mapalala**. Sista huyu alikuwa sista wa shirika la Mabinti wa Maria. Alikuwa mtoto wa katekista Benard Mapalala ambaye baadaye alihamishiwa parokia ya Usongo.Kwa bahati iliyoje, Sista Maria Claudia Mapalala aliyekuwa na vipaji vingi katika sanaa na muziki, alibahatika pia Kuwa mama mkuu wa shirika nchini mwaka 1988-1993.

Hao ni baadhi tu ya waliojitwalia sifa za pekee kama wanufaika wa umisionari toka hapa kwetu Ndala. Ni wazi kwamba hata wengine pia wote walifanya mambo mengi mazuri na kuiwakilisha vizuri parokia yetu. Hao wachache watoshe kuwakilisha wengine ili tuone ni namna gani umisionari ulizaa matunda chanya kwa namna ya pekee kabisa hapa kwetu Ndala.

## Padre Athanas Kiyenze

Padre Athanas kiyenze ni mzaliwa wa kijiji chaMangashini kilichokuwa katika parokia ya Ndala wakati huo na kigango cha Tongi ambayo sasa ni parokia pia. Wazazi wake ni, Baba katekista Gervas Ndulila na mama ni Auleria Hoka.

Makatekista waliokua wanufaika wa mwanzo kabisa wa imani hii yaani Ukristo hawakuwa nyuma pia katika kuhimiza maisha ya wakfu. Tunaona kwamba mapadre wengi wa mwanzo walikuwa ni watoto wa makatekista hao. Hii inaonyesha jinsi walivyokuwa mstari wa mbele si kwa kuhimiza wengine tu bali walianza katika familia zao wao wenyewe.

Pamoja na hamasa ya moja kwa moja toka kwa wamisionari lakini pia Baba (Katekista Gervas) alikuwa mstari wa Mbele katika kumpa ushirikiano juu ya chachu iliyowekwa na wamisionari Ndani mwake. Ndio kusema kwa hamasa hiyo aliweza kujiunga na malezi hayo ya Upadre kwa kufuata vyema masomo na taratibu husika.

Alipohitimu masomo yote, Ndiposa mnamo tarehe 01/08/1971 akapatiwa Daraja Takatifu ya Upadre. Anasema kwamba ili kuwa na ushiriki chanya wa ndugu jamaa na marafiki kwa wakati ule ilifaa sana tukio hilo(Upadrisho) lifanyike mazingira ya karibu na nyumbani. Hii ilikuwa ni kutokana na uduni wa miundombinu hali ambayo ingezuia kundi kubwa la watu kushiriki kama ingefanyikia parokiani (Ndala) kutokana na umbali.

Kutokana na hayo yote ililazimu basi kuangalia kigango cha karibu na nyumbani(Tongi) na huko ndipo alikopatiwa zawadi hiyo ya Daraja Takatifu ya Upadre. Ndio kusema pamoja na Tongi kuwa parokia sasa, tunamtazama baba yetu huyu kama mzaliwa wa Ndala kwani ndivyo ilivyokuwa wakati huo.

Kwa kuadhimisha jubilii ya dhahabu Padre Athanas Kiyenze anazidi kuwa hodari katika rika la wazee sio kwa umri pekee bali pia kwa uzoefu wa kazi ndani ya kanisa Katoliki kama padre. Tunaamini kabisa mafanikio yake kwenye utume ndani ya kanisa yana mchango mkubwa toka kwa wazazi wake, ndugu zake, jamaa na marafiki zake. Hivyo anatualika sote wenye mapenzi mema kumuambia Mungu ahsante kwa neema zake wezeshi kwa kipindi chote cha utume wake anaoendelea nao kama Padre.

## ORODHA YA MAPAROKO WA PAROKIA YA NDALA

### A. WAMISIONARI (WHITE FATHERS)

| JINA | MUDA (MWAKA) |
|---|---|
| 1. Fr. Antoon Van der Wee | Jan. 1896-Sept. 1895 |
| 2. Fr. Charles Desoignies | Sept. 1896-April 1898 |
| 3. Fr. Franz Muller | April 1898-Aug. 1901 |
| 4. Fr. Antoon Van der Wee | Aug. 1901-March 1904 |
| 5. Fr. Guillaume Schregel | March 1904-Aug. 1907 |
| 6. Fr. Antoon Van der Wee | Aug. 1907-Dec. 1908 |
| 7. Fr. Pierre Bedbeder | Dec. 1908-Dec. 1910 |
| 8. Fr. Guillaume Schregel | Dec. 1910-Aug. 1919 |
| 9. Fr. Jan Meeuwsen | Aug. 1991-Aug. 1921 |
| 10. Fr. Fridolin Boesch | Aug. 1921-Dec. 1921 |
| 11. Fr. Henri de Langle | Dec. 1921-Nov. 1927 |
| 12. Fr. Harrie Van der Eerden | Nov. 1927- 1934 |
| 13. Fr. Gerard Horsten | 1934- 1934 |
| 14. Fr. Fridolinv Boesch | 1934- 1945 |
| 15. Fr. Jean-Baptiste Cuierrier | 1945- ____ |
| 16. Fr. Frederic Debets | ___ - Jan. 1964 |
| 17. Fr. Joseph de Rooije | Jan. 1964- 1982 |
| 18. Fr. Josef Roes | 1982- 1993 |
| 19. Fr. Frank Nolan | 1993- 2002 |

### B. WAZALENDO

| JINA | MUDA (MWAKA) |
|---|---|
| 20. Fr. DeogratiasShiwala | April 2002- March 2008 |
| 21. Fr. Leons Maziku | March 2008-Aug. 2008 |
| 22. Fr. Daniel Malingumu | Aug. 2008- Jan. 2009 |
| 23. Fr. Nicholaus Bulabuza | Jan. 2009- Aug. 2014 |
| 24. Fr. Peter Bugumba (*Kaimu Paroko*) | Aug. 2014-Nov.2015 |
| 25. Fr. Focus S. Ruzoka (*Kaimu Paroko*) | Nov.2015-Juni 2016 |

26. Fr. Nicholaus J. Bulabuza Juni 2016-May 2017
27. Fr. Patrick Msekwa May 2017-Okt. 2018
28. Fr. Alex Nduwayo Okt. 2018-

Utafitina Fr. Focus ShukuruRuzoka
Jubilei ya Miaka 125 ya Ukristo Parokia ya Ndala (30/10/2021)

**TAKWIMU ZA WABATIZWA**

| **MWAKA** | **WABATIZWA** | **COM 1** | **KIPAIMARA** | **NDOA** |
|---|---|---|---|---|
| **2020** | **218** | | **74** | **25** |
| **2021** | **532** | | **261** | **81+6= 89** |

**Wabatizwa wa kitabuni mpaka sasa 40,487.**

**KUMBUKUMBU YA JUBILEI YA MIAKA 125 YA PAROKIA YA NDALA.**

1. Mwanzoni mwa mwaka huu, tulianza maandalizi ya Jubilei ya parokia yetu ambapo tulilenga kuhuisha maisha ya kiroho na watu wengi kurudia maskramenti. Pia kijamii tulidhamiria kuanza ujenzi wa Sekondari tukianza kukarabati majengo yalikuwa ya wanafunzi wa utawa wa Mabindti wa Maria. Tunakushukuru Baba Askofu Mkuu wa kuweka jiwe la Msingi leo tarehe 30/10/2021.

   Tokea kikao chetu cha Halimashauri parokia kilipopitisha hayo, tulianza kuchangia na sasa wengi tumeona kazi hii inayoendelea.

   Mhashamu Baba za Askofu Mkuu Paul Ruzoka, Wageni wetu wote, Waamini wote na wote wenye mapenzi mema tunaomba mutuunge mukono. Tunahitaji kukusanya Shilingi milioni 514 hivi ilikuweza kukarabati mabweni na kujenga mengine, pia kujenga Maabara, Vyoo, madarasa zaidi, Bwalo, viwanja vya michezo na Uzio. Kwa awamu hii tuliyo nayo tunakusanya milioni 150 ambayo hii itatuwezesha kukamilisha majengo ya wali ili shule iweze kuanza.

   Naomba kila mmoja wetu hapo aunge mkono, tunatarajia ianze mapema iwezekanavyo ndani ya mwaka mmoja kuanzia sasa kwa uwezeshaji wenu.

2. Sherehe ya padre Athanasi Kiyenze, kwa kufikisha miaka 50 ya utume katika Altare ya Bwana. Padre Hongera sana.
3. Kuzindua Jubilei ya Miaka 25 ya Upadre Padre Joseph Maziku Kitebi, ambapo mwakani tuadhimisha Jubilei ya fedha ya huduma katika kanisa.

4. Mwisho ilikuwa ni kupima maeneo yetu na tuweze kupatiwa hati miliki. Haikuwa kazi rahisi, nashukuru sana Baba Askofu Mkuu Paulo Ruzoka na Ofisi yake, Taasisi tunazo pakana nazo, majirani, Viongozi wa Parokia na wazee na viongozi wastaafu akina Morisi na Ndamo ambao waliwezesha kupatikana. Na sasa tumefanikiwa kupima maeneo yote ya Kanisa katika hati tano kulingana na Matumizi. Asante Ofisi ya Mkurugenzi Nzega na vitengo vyote na serikali kwa Ujumla. Naomba nikubaidhi hati hizi baba Askofu Mkuu maana ni mali yako.

Asanteni sana kwa kunisikliliza.

JIMBO KUU KATOLIKI TABORA

PAROKIA YA MT JOSEPH BABA MLISHI WA YESU NDALA

**TAARIFA FUPI YA PAROKIA**

Tumsifu Yesu kristo …………………………………………

Mhashamu Baba Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Tabora Paulo Ruzoka, padre wetu mjubilee Padri Atanasi Kiyenze, Padri wetu unayezindua Jubilee ya miaka 25 padri Joseph Kitebi.

Awali ya yote tunamshukuru Mungu kwa tutufikisha siku ya leo ambayo ni ya kihistoria katika Parokia yetu tukiwa na matukio makubwa matatu

Kwanza tunamshukru mungu kwa zawadi ya padre Atanasi Kiyenze, Ambaye siku ya leo anamshukuru mungu kwa kufikia miaka Hamsini ya Upadri. Pili tunamshuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya Padri Joseph kitebi ambaye siku ya leo anazindua Jubilee ya miaka Ishirini na tano katika utume

Pia tunamshukuru mungu kwa siku ya leo Parokia yetu Inatimiza miaka 125 tangu kuanzishwa.

Mhashamu Baba Askofu Mkuu Parokia yetu inajumla ya vigango 28 vyenye jumla ya waumini 9,588 ambao ni wabatizwa. Siku ya leo Wanaparokia wote tunayo furaha kusherehekea sikuku ya parkia yetu tukiwa na malengo ya kujenga shule ya sekondari ya parokia lengo hili tulianza kulijadili katika vikao vyetu na tulikubaliana kuanza kujenga kwa awamu awamu. Ikiwa awamu ya kwanza tunatarajia kukusanya kiasi cha shilingi million mia moja hamsini (150,000,000/=) tukiwa na lengo la kukamilisha majengo yafuatayo.

- Madarasa sita
- Jengo la utawala
- Maktaba
- Maabara
- Mabweni mawili pamoja na kuanza msingi wa bwalo la chakula

Mhashamu Baba Askofu Mkuu leo tunapofikia kilele cha sherehe za jubilee tunakuomba uweke jiwe la msingi katika ujenzi wetu na kubariki majengo.

Mwisho tunawashukuru wageni wote mliofika na mliotuunga mkono katika shughuli zote za ujenzi na tunasema karibuni sana tusherekee pamoja na tunawaomba muendelee kutuunga mkono kwani mpaka sasa michango inayotarajia kukusanywa bado hatujafika hata robo, michango bado tunahitaji

Asanteni sana na karibuni sana Parokia ya Ndala